MFUKO WA
ELIMU
Jarida la Nane la Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA)

www.tea.or.tz | Oktoba - Desemba | 2025

USHIRIKIANO WA TEA NA UNICEF WAINUA UFAULU WA SAYANSI SHULE ZA SEKONDARI



- TEA YAIMARISHA TIMU YA WATAALAM WA MIRADI KUBORESHA UTEKELEZAJI. UK. 4
- VIJANA 230 KUNUFAIKA NA MRADI WA IPOSA KIGOMA. UK. 7

"Changia Mfuko wa Elimu, Boresha Miundombinu Ya Elimu"

KUHUSU TEA

Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) ni Taasisi ya umma iliyoanzishwa kwa Sheria ya Bunge ya Mfuko wa Elimu Na. 8 ya 2001 chini ya kifungu cha 5 (1) ili kuratibu na kusimamia Mfuko wa Elimu, ulioanzishwa kwa sheria hiyo hiyo. Sheria hiyo ilifanyiwa marekebisho mwaka 2013.

Madhumuni ya Mfuko wa Elimu ni kuongeza nguvu za Serikali katika kugharimia miradi ya elimu ili kuinua ubora wa elimu na upatikanaji wake kwa usawa, katika ngazi zote za Elimu kwa Tanzania Bara na Elimu ya Juu kwa Tanzania Zanzibar.



DIRA

Kuwa Mfuko wa Elimu bora wenye hadhi ya kimataifa unao tatua changamoto za elimu nchini, kwa kutumia vyanzo mbalimbali vya mapato katika kuchangia maendeleo endelevu nchini.



DHAMIRA

Kutafuta rasilimali fedha na vifaa kwa ajili ya Mfuko wa Elimu na kuzigawa rasilimali hizo kwa ufanisi katika kufadhili miradi ya elimu ili kuboresha upatikanaji wa elimu bora na ujuzi kwa usawa.

YALIYOMO

SALAAM ZA MKURUGENZI MKUU.....iii

USHIRIKIANO WA TEA NA UNICEF WAINUA UFAULU WA SAYANSI SHULE ZA SEKONDARI.....01

TEA YAIMARISHA TIMU YA WATAALAM WA MIRADI KUBORESHA UTEKELEZAJI.....04

DKT AKWILAPO AAGWA TEA.....05

SHULE SHIKIZI MBIZI YALETA CHACHU YA ELIMU KAKONKO.....06

UWEKEZAJI KATIKA UJUZI: VIJANA 230 KUNUFAIKA NA MRADI WA IPOSA KIGOMA 07

MAPINDUZI YA USAFI SHULENI: WANAFUNZI 831 KILOLELI WANUFAIKA 08

TEA NA MOHAMED ENTERPRISES WAJADILIANA NAMNA YA KUINUA UJUZI WA WATUMISHI.....09

TEA NA UNICEF WAFIKISHA MIRADI YA ELIMU VISIWANI ZANZIBAR.....10

KICHEMA SEKONDARI – SUMBAWANGA YANUFAIKA NA BWENI LA WASICHANA.....11

TIMU YA UHARIRI

Mwenyekiti: Masozi Nyirenda

Mhariri: Bestina Magutu

Wachangiaji: Eliafile Solla

Joyce Minja

ANUANI:

Mamlaka ya Elimu Tanzania(TEA)

S. L.P 2516, Dodoma- Tanzania

Barua pepe: info@tea.or.tz,

Tovuti www.tea.or.tz,

Instagram: Officialteatz,

SALAMU ZA MKURUGENZI MKUU



Uwekezaji, Ushirikiano na Uboreshaji wa Elimu: Mafanikio Yakiendelea Kupitia Mfuko wa Elimu wa Taifa unaosimamiwa na Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA)"

Karibu katika Toleo la Nane la Jaraida la Mfuko wa Elimu. Katika Jarida hili tutaona namna sekta ya elimu nchini inavyoendelea kupata chachu ya maendeleo kupitia uwekezaji wa kimkakati katika miundombinu, ujuzi na fursa za kielimu kwa watoto na vijana.

Kupitia Mfuko wa Elimu wa Taifa unaosimamiwa na Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo wakiwemo UNICEF Tanzania na Serikali ya Canada, miradi mbalimbali imeendelea kubadili maisha ya jamii kwa kuimarisha miundombinu ya elimu katika maeneo yenye uhitaji mkubwa.

Miongoni mwa mafanikio makubwa yanayoonekana ni uwekezaji katika miundombinu ya masomo ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati (STEM), hususan ujenzi na ukarabati wa maabara za sayansi pamoja na uboreshaji wa mazingira rafiki ya kujifunzia kwa vitendo. Miradi hii iliyotekelzwa katika mikoa ya Songwe, Kigoma na Tabora imeanza kuzaa matunda kwa kuongezeka kwa hamasa ya wanafunzi kuchagua masomo ya sayansi, kuboreshwa kwa ufaulu, na hivyo kuandaliwa kwa kizazi chenye ujuzi na ubunifu kinachoweza kushindana katika uchumi wa kisasa unaotegemea sayansi na teknolojia.

Aidha, ujenzi wa madarasa uliowezesha kuanzishwa kwa shule shikizi katika maeneo yaliyokuwa hayana huduma za shule umeleta mafanikio makubwa, ikiwemo ongezeko la udahili na upatikanaji wa huduma za elimu karibu na jamii.

Ili kuendelea kutoa huduma kwa ufanisi na ubora, Mfuko wa Elimu wa Taifa umeimarisha timu ya wataalam wa miradi, wakiwemo wahandisi, wasanifu majengo na wakadiriaji wa gharama za ujenzi, hatua inayohakikisha utekelezaji wa miradi unafanyika kwa weledi, ubora na uwazi.

Hatua hizi zinathibitisha dhamira ya TEA ya kuhakikisha upatikanaji wa elimu bora, salama, jumuishi na yenye tija kwa maendeleo ya taifa.

Dkt. Erasmus F. Kipesha
Mkurugenzi Mkuu-TEA

1.MAPINDUZI YA STEM: USHIRIKIANO WA TEA NA UNICEF WAINUA UFAULU WA SAYANSI SHULE ZA SEKONDARI

Katika kipindi hiki ambacho dunia inaongozwa na mapinduzi ya sayansi na teknolojia, uwekezaji katika masomo ya Sayansi, Teknolojia na Hisabati (STEM) ni nguzo muhimu ya maendeleo ya taifa. Kwa kulitambua hilo, Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), chini ya ufadhili wa Serikali ya Canada, wamekuwa wakitekeleza miradi ya pamoja ya kuimarisha miundombinu ya maabara za sayansi katika shule za sekondari mikoa ya Kigoma, Songwe na Tabora.

Miradi hiyo imetekelezwa katika awamu mbili kuanzia Mwaka wa Fedha 2023/2024 ambapo katika awamu ya kwanza jumla ya Sh milioni 344,232,700 zilitumika katika Ujenzi, umaliziaji na ukarabati wa jumla ya maabara tisa jumla ya maabara (9) katika mikoa hiyo ya Kigoma, Tabora na Songwe. Katika awamu ya pili iliyoanza kutekelezwa mwaka 2024/2025 kiasi cha Sh. Milioni 936.7 zimetumika kufadhili ujenzi, ukamilishaji na ukarabati wa vyumba vya maabara za sayansi vipatavyo 44 katika shule 20 za mikoa ya Songwe, Tabora na Kigoma.

Shule ya Sekondari ya Wasichana Kakonko, ni miongoni mwa shule zilizonufaika na ufadhili huo. Shule hiyo ambayo mwaka 202 kwa mara ya kwanza tangu kuanzishwa kwake ilipata wahitimu wa kidato cha nne imeelezea manufaa makubwa yaliyotokana na ufadhili wa ujenzi wa maabara tatu za sayansi kwa ajili ya masomo ya Kemia, Biolojia na Fizikia hasa ikizingatiwa kuwa shule hiyo ni ya mchepuo wa masomo ya sayansi.

Makamu Mkuu wa shule hiyo, Bw. Alex Lugaji Kagoma anasema, maabara hizo zimeleta mabadiliko makubwa kitaaluma. *“Wahitimu wetu wa kwanza 58 wamefaulu kwa viwango vya juu; sita wamepata Daraja la Kwanza, 42 Daraja la Pili na tisa Daraja la Tatu. Hakuna aliyepata Daraja la Nne wala Sifuri,”* anafafanua.

Anaongeza kuwa, maabara hizo zimewawezesha wanafunzi kujifunza kwa vitendo na kuwapa walimu nyenzo bora, rafiki na rahisi za kufundishia.

Mafanikio hayo yanafanana na yale ya Shule ya Sekondari Itumba iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Ileje mkoani Songwe ambapo, ukamilishaji wa maabara mbili za sayansi umeongeza idadi ya wanafunzi wanaochagua mkondo wa sayansi. Bw. Deogratius Asigile Msusa Makamu Mkuu wa shule hiyo anaeleza kuwa, mwitikio wa wanafunzi umeongezeka kwa kiasi kikubwa ikilinganishwa na kipindi cha nyuma ambapo shule ilikua haina maabara za sayansi.

Kwa upande wake Mkuu wa Shule ya Sekondari Nkangamo iliyopo Wilayani Momba mkoani Songwe Bw. Geofrey Mwakajila anasema, kabla ya ukarabati wa maabara tatu za sayansi, idadi ya wanafunzi waliokuwa wakijiunga na mchepuo wa masomo ya sayansi haikuzidi kumi. Hata hivyo, baada ya maboresho hayo na kuanza kwa mtaala mpya unaowapa wanafunzi fursa ya kuchagua masomo kuanzia kidato cha kwanza idadi hiyo imeongezeka kwa kiasi kikubwa.

Katika mwaka wa fedha 2023/2024, TEA kwa kushirikiana na UNICEF ilitekeleza miradi 13 yenye thamani ya Shilingi milioni 854. Aidha, katika mwaka wa fedha 2024/2025, miradi 35 yenye thamani ya Shilingi bilioni 1.55 ilitekelezwa, ikihusisha ujenzi na ukarabati wa maabara za sayansi, vyumba vya madarasa, na matundu ya vyoo katika mikoa ya Tabora, Songwe, na Kigoma.

Katika Shule ya Sekondari Kamagi iliyopo Wilayani Sikonge mkoani Tabora nayo pia ilipata ufadhili wa ujenzi wa maabara za Biolojia na Kemia. Wanafunzi wanachama wa Klabu ya STEM wanaonesha ari mpya ya kujifunza kwenye miundombinu hiyo iliyoboreshwa. Wanafunzi Magreth Mayunga Mlolasa (Kidato cha IV) na Nadia Abubakar Mwingireza (Kidato cha I) wanasema wamechagua masomo ya sayansi kwa kuwa yatawapa fursa ya kujiajiri na kutimiza ndoto zao za kitaaluma.

Magreth anaeleza kuwa, anatamani kuwa mfamasia na kuanzisha biashara yake ya kuwa na duka la kuuza dawa pamoja na kutoa ushauri wa kiafya badala ya kutegemea ajira.

Mwalimu wa Kemia na Biolojia katika shule hiyo Bw. Kassim Issa Mgayo anathibitisha kuwa, uwepo wa maabara hizo umeongeza hamasa kwa wanafunzi wengi wanaojiunga na shule hiyo kuchagua mkondo wa sayansi. Anafafanua kuwa, idadi kubwa ya wanafunzi waliojiunga kidato cha kwanza wameonyesha nia ya kujiunga na mkondo wa masomo ya sayansi. Kwa vile mtaala mpya wa elimu kwa sasa unaelekeza wanafunzi kuanza kuchangua mkondo wa masomo wanayotaka, idadi kubwa ya wanafunzi wa kidato cha kwanza wanajiunga na masomo ya sayansi amesema Mwalimu Mgayo.

Shule nyingine za Sekondari zilizonufaika na miradi ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya STEM ni pamoja na Shule ya Sekondari Kashoza (Kakonko), Gwanumpu (Kakonko), Migezi (Kibondo), Rugenge (Kakonko), Busami (Kibondo), Nyamidaho (Kasulu), Nyakitonto (Kasulu) Mount Samba (Kibondo) Masanga (Kigoma) zilizoko Mkoani Kigoma.

Katika mkoa wa Tabora shule nyigine zilizonufaika ni pamoja na Dkt. J.P. Magufuli (Kaliua), Goweka (Uyui), Langwa (sikonge), Ngulu (Sikonge), Kizengi (Uyui), Pangale (Sikonge) na Usagali (Uyui). Kwa upande wa Songwe shule za sekondari zilizonufaika ni Bupigu (Ileje), Shiwinga na Ndugu zote za Mbozi.

Kwa ujumla, miradi hii ya pamoja imelenga kuweka mazingira wezeshi ya ufundishaji na ujifunzaji wa masomo ya STEM nchini, hatua inayochangia kuandaa kizazi chenye maarifa, ujuzi na ushindani katika dunia ya sasa ya sayansi na teknolojia

Sekta ya elimu nchini inazidi kupata chachu ya maendeleo kupitia miradi ya kuimarisha miundombinu, ujuzi na fursa za kielimu kwa watoto na vijana. Katika mikoa mbalimbali, Mfuko wa Elimu wa Taifa unaosimamiwa na TEA kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo UNICEF Tanzania na Serikali ya Canada, imeendelea kubadilisha maisha ya jamii kwa kuimarisha miundombinu ya elimu.

Miongoni mwa miradi ya ushirikiano iliyoleta mafanikio makubwa ni ule wa Kijiji cha Mbizi Wilayani Kakonko mkoani Kigoma, ambapo TEA, UNICEF na Serikali ya Canada wamewezesha ujenzi wa madarasa yaliyopelekea kuanzishwa kwa shule shikizi. Kwa kipindi kifupi, jumla ya wanafunzi 500 wameandikishwa shuleni hapo na kupata fursa ya elimu ya awali hadi darasa la tano bila kutembea umbali mrefu waliokuwa wakilazimika kutembea hapo awali. Mafanikio haya yametoa motisha kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko kujenga madarasa mengine nane, matundu 16 ya vyoo na ofisi ya walimu ili kuboresha miundombinu ya shule na mazingira ya kujifunzia.


Zaidi ya hayo, TEA imeimarisha timu ya wataalam wa miradi ikiwemo wahandisi, msanifu na mkadiriaji wa gharama za ujenzi kwa lengo la kuhakikisha miradi inayotekelezwa kupitia Mfuko wa Elimu wa Taifa inafanikishwa kwa weledi, ubora na uwazi. Hii inajumuisha miradi kama vile Vituo vya Ufundi wa Awali (IPOSA) vinavyolenga kutoa mafunzo ya ujuzi kwa vijana walio nje ya shule katika mikoa ya Tabora, Kigoma, Songwe, Dar es Salaam na Dodoma ambapo zaidi ya vijana 800 wanatarajiwa kunufaika na mafunzo ya ujuzi, ufundi stadi na kompyuta ili waweze kukuza ajira binafsi na ustawi wa kiuchumi.

Shule nyingine pia zimepata maboresho makubwa kama vile: Shule ya Msingi Kilolelili ya mkoani Tabora ambayo imefaidika na ujenzi wa matundu 10 ya vyoo kwa ufadhili wa UNICEF, Serikali ya Canada kwa kushirikiana na TEA, Shule ya Sekondari Dkt. John Pombe Magufuli iliyopo Wilayani Kaliua mkoani Tabora, iliyonufaika na ujenzi wa maabara ya Kemia ambayo imechochea hamasa ya wanafunzi kusoma masomo ya sayansi.

Zaidi ya kujenga na kuboresha miundombinu, TEA imeendelea kushirikiana na sekta binafsi kuweka mikakati ya kuwaongezea watumishi ujuzi mahala pa kazi. Katika kulifanikisha hili TEA na Mohamed Enterprises Tanzania Limited (MeTL Group) walikutana na kujadiliana jinsi gani wanaweza kushirikiana kupitia Mfuko wa Kuendeleza Ujuzi kama sehemu ya kuwapa motisha, kukuza uwezo na kuwaongezea maarifa zaidi ya utekelezaji wa majukumu yao.

Miradi hii yote inathibitisha dhamira ya TEA kuhakikisha upatikanaji wa elimu bora, salama, jumuishi na yenye tija.





2. TEA YAIMARISHA TIMU YA WATAALAM WA MIRADI KUBORESHA UTEKELEZAJI

Katika kuimarisha usimamizi na utekelezaji wa miradi ya elimu, Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) imeongeza wataalam wanne katika timu yake ya miradi wakiwemo wahandisi wa ujenzi wawili, msanifu majengo mmoja na mkadiriaji wa gharama za ujenzi mmoja.

Hatua hii inalenga kuboresha ufanisi katika usimamizi wa miradi inayotekelezwa kupitia Mfuko wa Elimu wa Taifa unaosimamiwa na TEA.

Akizungumza kuhusu maendeleo hayo Meneja wa Miradi ya Elimu Bi. Mwafatuma Mohamed amesema ujio wa wataalam hao utaimarisha zaidi zoezi la upitiaji, usanifu na usimamizi wa miradi.

Ameeleza kuwa hapo awali TEA ilikuwa ikitegemea wataalam kutoka nje, wakiwemo wa halmashauri na taasisi nyingine za umma, hali iliyokuwa ikipunguza kasi ya utekelezaji wa miradi endapo wataalam hao wangekuwa na majukumu mengine katika taasisi zao.

Kwa sasa miradi yote inasimamiwa na wataalam wa ndani ambao wanashirikiana na wataalam kwenye halmashauri nufaika hivyo kufanya Utekelezaji kuwa na ufanisi na ubora zaidi. Aidha, ameongeza kuwa uwepo wa mkadiriaji wa gharama unasaidia kupata makadirio sahihi ya gharama za ujenzi na hivyo kuongeza uwazi na ufanisi katika matumizi ya rasilimali.

Akizungumzia matarajio ya taasisi Bi. Mohamed amewahimiza wataalam hao kufanya kazi kwa bidii, weledi na kuzingatia maslahi ya umma akisisitiza umuhimu wa kudumisha ubora wa miradi inayotekelezwa kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo.

Kupatikana kwa wataalam hao kunatarajiwa kuongeza ubora wa utekelezaji wa miradi ya TEA na kusaidia miradi hiyo kukamilika kwa wakati na kwa viwango vinavyokubalika.

Kwa upande wake Mhandisi Moses Tubanga amesema, jukumu lake yeye pamoja na wataalam wenzake ni kuhakikisha miradi inayotekelezwa kupitia Mfuko wa Elimu wa Taifa inakuwa na ubora unaokidhi viwango vinavyotakiwa na matarajio ya wadau wa maendeleo ya sekta ya elimu.

Naye msanifu majengo Bi. Prisca Kalungula ameeleza kuwa, jukumu lake ni kuandaa michoro na ramani za miradi ili kuhakikisha zinazingatia vigezo vya kitaalamu na miongozo mbalimbali ya ujenzi inayotolewa na Serikali kabla ya utekelezaji wake



Timu ya Wakandarasi kutoka Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), wakipitia na kuandaa michoro kwa kushirikiana na wadau kutoka Shirika la Maendeleo la Korea (KOICA), kwa ajili ya Ujenzi wa maabara za Sayansi na TEHAMA

3. DKT AKWILAPO AAGWA TEA

Batika Bodi na Menejimenti ya Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) Novemba 14, 2025 walimuaga rasmi aliyekuwa Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Mhe. Dkt. Leonard Akwilapo ambaye kwa sasa ni Mbunge wa Jimbo la Masasi Mjini kufuatia ushindi alioupata katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 29, 2025, kisha kuteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Akizungumza kwa niaba ya Bodi na Menejimenti Makamu Mwenyekiti wa Bodi Bw. Elirehema Mollel amempongeza Dkt. Akwilapo kwa kushinda kwenye uchaguzi mkuu na kusema, ushindi huo ni ishara ya kuaminiwa na wananchi kwa uadilifu na weledi wake.

Bw. Mollel aliongeza kuwa, misingi imara iliyojengwa na Dkt. Akwilapo itaendelea kuwa mwongozo wa utekelezaji wa majukumu ya TEA kwa sasa na baadaye. Alisisitiza kuwa, mchango wake umeleta matokeo chanya katika uboreshaji wa miundombinu ya elimu na kuongeza ufanisi katika utafutaji wa rasilimali fedha na vifaa kwa maendeleo ya elimu. “Daima tutakukumbuka kwa maono yako na uongozi uliotujengea. Tunakutakia kila la kheri katika majukumu yako mapya,” alisema.

Kwa upande wake Dkt. Akwilapo, aliishukuru Bodi na Menejimenti ya TEA kwa ushirikiano wa karibu alioupata wakati wote wa uongozi wake. Alisema kwamba, mafanikio yaliyopatikana yametokana na umoja, ushirikiano, nidhamu na moyo wa kujituma kati ya Bodi, Menejimenti na wtumishi wote kwa ujumla.

Aidha, Dkt. Akwilapo aliahidi kuendelea kushirikiana na TEA kupitia nafasi yake bungeni, kwa kuisemea vyema ili kufanikisha utekelezaji wa miradi zaidi kwa lengo la kuongeza upatikanaji ubora wa elimu na kwa usawa.

Wakati huo huo Watumishi wa Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) wamefanya hafla fupi ya kumuaga mtumishi mwenzao, Bi. Maria Masanja, aliyemaliza rasmi safari yake ya utumishi wa umma baada ya kutumikia TEA kwa zaidi ya miaka 14. Katika hafla hiyo, watumishi wa TEA wamemuelezea Bi. Maria kama mtu mkarimu, mwenye heshima na moyo wa upendo. Alijulikana kwa utayari wake wa kuwakarimu watumishi wapya na kuwafanya wajisikie nyumbani muda wote wa utumishi wao.

Watumishi wamemtakia afya njema, baraka na maisha mema katika ukurasa wake mpya wa maisha ambapo atakumbukwa daima kwa uchapakazi, unadhifu na tabasamu lake la faraja kwa wengi.



Aliyekuwa Mwenyekiti wa Bodi ya TEA Dkt. Leonard Akwilapo (katikati) akiwa kwenye picha yta pamoja na Wajumbe wa Bodi hiyo mara baada ya kikao maalumu cha kuagana nao.



Aliyekuwa Mwenyekiti wa Bodi ya TEA Dkt. Leonard Akwilapo (katikati) akitoka nje ya jengo la TEA mara baada ya kuagana na Wajumbe wa Bodi na Menejimenti wa TEA. Kushoto ni Makamu Mwenyekiti wa Bodi Bw. Elirehema Mollel na kulia ni Mkurugenzi Mkuu wa TEA Dkt. Erasmus Kipesha.

4. SHULE SHIKIZI MBIZI YALETA CHACHU YA ELIMU KAKONKO

Uwekezaji katika miundombinu ya elimu unaendelea kuleta matokeo chanya nchini. Katika Kijiji cha Mbizi, Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko mkoani Kigoma, idadi ya wanafunzi walioandikishwa imeongezeka kutoka wanafunzi 50 waliokuwa wamesajiliwa mwaka 2024/2025 hadi wanafunzi 500 mwaka 2025/2026, baada ya kupatikana kwa ufadhili wa ujenzi wa madarasa kupitia Mfuko wa Elimu wa Taifa. Wanafunzi hao 500 ni wa kuanzia ngazi ya awali hadi darasa la tano.

Akizungumzia maendeleo hayo, Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Bw. Wilfred William, amesema mradi huo uliotekelezwa kwa gharama ya Sh. 35,668,750 umeleta hamasa kubwa kwa wazazi kuwasajili watoto wao, hususan katika elimu ya awali.

Kabla ya ujenzi huo, watoto wa Kijiji cha Mbizi walilazimika kutembea umbali wa takribani kilometa nane kufuata huduma ya shule, hivyo, uwepo wa shule hiyo mpya umeondoa changamoto hiyo na kuongeza fursa kwa watoto wengi kupata elimu kwa urahisi.

Kutokana na mafanikio ya awali ya mradi huo, Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko imeongeza juhudi kwa kujenga madarasa mengine nane (8), matundu 16 ya vyoo pamoja na ofisi ya walimu, hatua inayoboresha miundombinu ya shule na mazingira ya kujifunzia.

Kwa upande wake, Meneja wa Miradi ya Elimu kutoka TEA, Bi. Mwafatuma Mohamed, amepongeza uongozi wa Halmashauri hiyo kwa usimamizi mzuri wa mradi huo na kumshukuru Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Bw. Stephen Mhilu, kwa juhudi zake katika kuhakikisha utekelezaji wa mradi unakamilika kwa wakati na kuwa na tija.

Aidha, imeelezwa kuwa wakati wa kuanza kwa mradi katika mwaka wa fedha 2024/2025, zaidi ya wanafunzi 50 wa elimu ya awali walikuwa wakipata masomo yao katika ofisi ya kijiji kutokana na ukosefu wa miundombinu ya shule. Hivi sasa, hali hiyo imebadilika kwa kiasi kikubwa.

Ushiriki wa wananchi wa Kijiji cha Mbizi katika kutoa eneo kwa ajili ya ujenzi wa shule hiyo ni kielelezo cha ushirikiano mzuri kati ya jamii na wadau wa maendeleo katika kuimarisha sekta ya elimu. Ujenzi wa mradi huo ni sehemu ya miradi ya ushirikiano kati ya TEA na UNICEF, kwa ufadhili wa Serikali ya Canada.





Madarasa kwa ajii ya Shulel Shikizi ya Mbizi- Kakonko- Kigoma

5. UWEKEZAJI KATIKA UJUZI: VIJANA 230 KUNUFAIKA NA MRADI WA IPOSA KIGOMA

Zaidi ya vijana 230 wanatarajiwa kunufaika na mafunzo ya ujuzi yatakayotolewa kupitia Vituo vya Ufundi wa Awali vinavyojihusisha na Mpango wa Elimu Changamani kwa Vijana Walio Nje ya Shule (IPOSA), kufuatia kukamilika kwa ujenzi wa vyumba vitatu vya madarasa katika Shule ya Msingi Makere, Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu mkoani Kigoma.

Mradi huo unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Mamlaka ya Elimu Tanzania na UNICEF, ukilenga kupanua fursa za elimu kwa vijana walio nje ya mfumo rasmi wa elimu.

Kituo hicho cha Ufundi wa Awali (IPOSA) kinalenga kutoa mafunzo ya ujuzi na ufundi stadi hususan katika fani za ushonaji na matumizi ya kompyuta ili kuwawezesha vijana kujiajiri, kuongeza kipato na kuboresha maisha yao kiuchumi.

Akizungumzia maendeleo ya mradi huo mwalimu wa shule ya msingi Makere Bw. Rashid Mbwile amesema, idadi ya vijana wanaotaka kujiunga kwenye Kituo hicho cha IPOSA ni kubwa hivyo kukamilika kwake kutapanua wigo wa udahili na kutoa fursa kwa vijana wengi waliokuwa wakisubiri nafasi kujiunga na mafunzo hayo ya ujuzi.

Kwa upande wake Msimamizi wa Miradi ya IPOSA kutoka TEA Bw. John Mtiba amesema, utekelezaji wa miradi hiyo unaendelea vizuri katika vituo vyote 10 vinavyojengwa na kuongeza kuwa anaamini miradi hiyo itakamilika kwa wakati na kuanza kutoa huduma kwa vijana.

Ameeleza kuwa, miradi hiyo ikikamilika yote itawawezesha zaidi ya vijana 800 kupata ujuzi katika fani mbalimbali, hatua itakayochochea ajira binafsi na kuwasaidia kujikwamua kiuchumi. Kwa ujumla, miradi 10 ya IPOSA inatekelezwa kwa thamani ya Shilingi bilioni moja katika mikoa ya Tabora, Songwe, Kigoma, Dodoma na Dar es Salaam.

Vituo vya IPOSA vinalenga kukidhi mahitaji ya kielimu kwa vijana walio nje ya mfumo rasmi wa elimu wakiwemo ambao hawakuwahi kujiunga na shule, walioacha shule katika ngazi mbalimbali pamoja na waliomaliza darasa la saba bila kuendelea na elimu ya sekondari. Aidha, uwepo wa chumba maalum kwa ajili ya wanafunzi wa kike wenye watoto wadogo unaonesha dhamira ya kuimarisha ujumuishi na usawa wa kijinsia katika elimu.



Muonekano wa jengo la Kituo cha Ufundi wa Awali chini ya Mpango wa Elimu Changamani kwa Vijana Walio Nje ya Shule (IPOSA) kinachojengwa Shule ya Msingi Makere iliyopo Mkoani Kigoma, Wilayani Kasulu,

6. MAPINDUZI YA USAFI SHULENI: WANAFUNZI 831 KILOLELI WANUFAIKA

Zaidi ya wanafunzi 831 wa Shule ya Msingi Kiloleli, wilayani Sikonge mkoani Tabora wamenufaika na ujenzi wa matundu 10 ya vyoo kupitia mradi wa pamoja wa Mamlaka ya Elimu Tanzania, Serikali ya Canada na UNICEF.

Mradi huo wenye thamani ya Sh. milioni 30 umelenga kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia na tayari umeleta nafuu kubwa kwa wanafunzi na walimu waliokuwa wakikabiliwa na changamoto ya uhaba wa vyoo shuleni hapo.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo Bw. Festo Ponela amesema, shule hiyo iliyoanzishwa mwaka 1974 na ilikuwa na matundu sita tu ya vyoo kwa wanafunzi zaidi ya 800 hali iliyosababisha msongamano mkubwa na kuhatarisha afya na usalama wa walimu na wanafunzi. Ameongeza kuwa, changamoto hiyo ilichangia ongezeko la utoro miongoni mwa wanafunzi hivyo kuathiri ukuaji wa taaluma shuleni hapo.

Kwa upande wake Rehema Usega akizungumza kwa niaba ya wazazi amesema, mradi huo umeleta mabadiliko makubwa kwenye shule hiyo na kwamba kwa sasa watoto wao wanasoma katika mazingira bora na salama zaidi.

Amebainisha kuwa awali baadhi ya wanafunzi walikosa masomo kutokana na changamoto ya vyoo, lakini hali hiyo imepungua kwa kiasi kikubwa baada ya kukamilika kwa ujenzi wa matundu mapya ya vyoo.

Mradi huu ni sehemu ya juhudi endelevu za TEA kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo katika kuhakikisha shule za msingi na sekondari nchini zinakuwa na miundombinu bora inayowezesha utoaji wa elimu salama, jumuishi na yenye tija kwa watoto wote wa Kitanzania.



Muonekano wa Matundu ya Vyoo yaliyojengwa kwa ufadhili wa UNICEF kwa kushirikiana na TEA shule ya Msingi Kiloleli iliyopo Wilayani Sikonge, Mkoani Tabora

7. TEA NA MOHAMED ENTERPRISES WAJADILIANA NAMNA YA KUINUA UJUZI WA WATUMISHI

Uongozi wa Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) Novemba 27, 2025, ulikutana na kufanya mazungumzo na Kampuni ya Mohamed Enterprises Tanzania Limited (MeTL Group) katika ofisi za TEA makao makuu yaliyopo Ilazo Extension Dodoma Novemba 7, 2025.

Lengo la kikao hicho lilikuwa kujadili namna ambavyo taasisi hizi mbili zinaweza kushirikiana katika kuwajengea watumishi uwezo mahala pa kazi kupitia Mfuko wa Kuendeleza Ujuzi (SDF), unaosimamiwa na TEA.

Timu ya TEA iliongozwa na Dkt. George Mofulu, Meneja Utafutaji Rasilimali na Hamasa, huku timu ya MeTL Group ikiongozwa na Mhandisi Ali Farooq, Meneja Miradi ya Mafunzo ya Ufundi Stadi.

Kabla ya mazungumzo hayo, timu ya MeTL Group ilipata nafasi ya kukutana na Mkurugenzi Mkuu wa TEA Dkt. Erasmus Kipesha ambaye aliwashukuru kwa utayari wao wa kushirikiana na TEA na kusisitiza kuwa yapo maeneo mengi yenye fursa za ushirikiano kwa ajili ya kuendeleza sekta ya elimu nchini.

Kwa upande wake Mhandis Ali Farooq, alitoa shukurani kwa niaba ya uongozi wa MeTL Group na kuahidi kuwa watayafanyia kazi makubaliano yote ili kuendelea kuinua kiwango cha elimu na ujuzi kwa Watanzania.



Mkurugenzi Mkuu wa TEA Dkt. Erasmus Kipesha akipokea zawadi kutoka kwa Meneja Miradi ya Mafunzo ya Ufundi Stadi wa MeTL Group Mhandisi Ali Farooq mara baada ya kikao cha pamoja cha kujadili maeneo ya ushirikiano.

8. TEA NA UNICEF WAFIKISHA MIRADI YA ELIMU VISIWANI ZANZIBAR

Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) kwa kushirikiana na UNICEF Tanzania wameanza rasmi utekelezaji wa miradi ya elimu visiwani Zanzibar kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali (WEMA), yenye lengo la kuboresha miundombinu ya shule na kutoa fursa kwa wanafunzi kujifunza kwenye mazingira na salama bora zaidi.

Kupitia ushirikiano huu, TEA na UNICEF wametenga jumla ya Shilingi Bilioni 2.5 kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa vyumba vya madarasa, maabara za sayansi pamoja na matundu ya vyoo katika shule 20 ambapo shule 11 zipo kisiwani Unguja na shule 9 kisiwani Pemba.

Akizungumza kwenye kikao maalum na timu kutoka Wizara ya Elimu - Zanzibar Mkurugenzi Mkuu wa TEA Dkt. Erasmus Kipesha alisema, utekelezaji unatarajiwa kuanza mwishoni mwa mwezi Januari na kukamilika kabla ya mwezi wa sita mwaka 2026. Alibainisha kuwa lengo ni kuwawezesha wanafunzi kusoma katika mazingira bora, salama na rafiki kwa afya zao.



Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Elimu Tanzania Dkt. Erasmus Kipesha akitoa maelezo kuhusu ufadhili wa miradi ya ukarabati na ujenzi wa miundombinu kwa shule za Unguja na Pemba visiwani Zanzibar.

Dkt. Kipesha pia alisisitiza kuwa, TEA kama taasisi ya Muungano ina wajibu wa kutekeleza miradi ya elimu Zanzibar na kuhakikisha miradi hiyo inaleta matokeo chanya kwa jamii.



Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Bw. Khamis Said akifafanua jambo katika kikao kazi maalum cha kujadili utekelezaji wa miradi ya elimu kupitia Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) visiwani Zanzibar.

Kwa upande wake Mkuu Katibu Mkuu - WEMA Bw. Khamis Said, aliishukuru TEA kwa mchango wake na kueleza kuwa miradi hiyo imechochea wadau wengine kuchangia maendeleo ya elimu.

Aliongeza kuwa ujenzi na ukarabati huo umefika wakati muafaka na ukikamilika utaleta mabadiliko chanya kwa shule na wanafunzi visiwani humo.

9. KICHEMA SEKONDARI – SUMBAWANGA YANUFAIKA NA BWENI LA WASICHANA

Bweni la wasichana katika Shule ya Sekondari Kichema iliyopo Manispaa ya Sumbawanga Mkoa wa Rukwa limekamilika na kuanza kutoa huduma kwa wanafunzi. Bweni hilo lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 80 limejengwa kwa fedha kutoka Mfuko wa Elimu wa Taifa unaosimamiwa na Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), ambapo kiasi cha shilingi milioni 120 kimetumika. Ujenzi wa bweni hilo umeboresha kwa kiasi kikubwa mazingira ya kujifunza kwa kupunguza adha ya wanafunzi kutembea umbali mrefu kila siku. Hatua hiyo imeongeza usalama, muda wa kujisomea pamoja na kuimarisha ufaulu wa kitaaluma.

Meneja Miradi wa TEA Bi. Mwafatuma Mohamed ameipongeza Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga kwa kusimamia vyema utekelezaji wa mradi huo na kuhakikisha bweni linakamilika kwa wakati na kutumika kama ilivyokusudiwa.



Bweni la wanaunzi wa kike katika Shule ya Sekondari Kichema Sumbawanga Mkoani Katavi

Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA)

P.O. Box 2516, Ilazo - Dodoma.

info@tea.or.tz www.tea.or.tz officialteatz

"Changia Mfuko wa Elimu, Boresha Miundombinu Ya Elimu"